# Ushairi wa Kiswahili kuanzia karne ya 16 mpaka karne ya 20

–

# Nadharia kuhusu Arudhi na Bahari za Kishairi

DL2A

SORBONNE PARIS CITÉ
RECHERCHE ENSEIGNEMENT SUPÉRIEUR

**Daktari Mathieu ROY**
**$DL_2A$ - Recherche**
**2014**

# Copyrighted materials

Haki zote zimehifadhiwa.

Picha zinazofuata zilitafsiriwa na Mathieu Roy kutoka tasnifu yake ya uzamivu (Kifaransa) inayopatikana bure ukibonyeza hapa.

- Utangulizi
- Arudhi ni nini?
- Bahari ni nini?

# Maendeleo ya Ushairi wa Kiswahili yalifuata mageuzo ya lugha ya Kiswahili katika uwanja mkubwa sana



# Nadharia kuhusu Ushairi zina asili tofauti zinazohitilafiana katika maelezo yake

- Miswada, vitabu na mashairi vya washairi wenyewe wakiandika kwa herufi za Kirumi au Kiajemi
- Vitabu vya mashairi yaliyokusanywa na watalaamu kutoka Ulaya
- Makala na vitabu kuhusu arudhi, kazi ya wanaisimu wa Vyuo Vikuu

# A. Hali ya hitilafu kati ya nadharia za Arudhi

# Vitabu kamili vya kwanza kuhusu Arudhi viliandikwa kwa Kiswahili

- Mwaka 1954, kitabu cha kwanza kudhihirisha sheria za arudhi kiliandikwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi (1924-1964) : *Sheria za kutunga mashairi*. KLB.

- 1988: *Tungo zetu* kilipigwa chapa na Ibrahim Noor Shariff katika New Jersey – Marekani. Red Sea Press.

# Hitilafu katika nadharia

a) Ushairi wa Kiswahili ulizaliwa wapi?
   - Katika sehemu za Kaskazini mwa lahaja za Kiswahili tu?
   - Au Kusini pia? Kilwa (Tanzania) ni mji wa kale uliosahauliwa katika historia ya sanaa ya ushairi

b) Lini?
   - Karne ya 9, 10, 11, 13, 16 au 18?

c) Kwa asili za kiutamaduni gani?
   - Nyimbo na ngoma za Kiafrika *au* Bahari za tamaduni ya Kiarabu au Kiajemi

# Katika vitabu kumbe sheria za kutunga mashairi na maelezo yanatofautiana sana

1) Msingi wa ushairi ni katika urefu wa silabi: ruwaza za ushairi wa kale wa Wagiriki, Waarabu na Waajemi zilitumiwa kueleza ushairi wa Kiswahili (karne ya 19 hadi 20)
2) Msingi wa ushairi ni kikazo katika silabi fulani kama katika ushairi wa Kiingereza au Kijerumani (1917, 2011)
3) Msingi wa ushairi ni silabi katika utungo wa vina na hesabu ya mizani (1954, 1988)
4) **Je na ukweli wake upo?**

# B. Nadharia na ukaguzi wake

# B. 1) Arudhi zinazoundwa na urefu wa silabi: Ruwaza za Wagiriki wa Kale katika Ushairi wa Kiswahili

- Iambic (Büttner, 1894):
  Mara mbili silabi fupi na ndefu ᴗ – (iamb) zaunda bahari ya mashairi
- Trochaic (Büttner, 1894):
  Mara mbili – ᴗ (trochée)
- Anapaestic (Steere, 1870):
  Mara mbili ᴗ ᴗ – (anapeste)
- Ionic (Allen **1971**):
  – – ᴗ ᴗ (ionic kuu)
  ou ᴗ ᴗ – – (ionic ndogo)

# B. 1. Ruwaza za Kiarabu na Kiajemi

# B. 1) Mwundo wa mstari au ubeti katika Ushairi wa Kiarabu wa kiutamaduni




Source : Georges BOHAS et Bruno PAOLI « Métrique arabe : une alternative au modèle xalilien » *in* (BOHAS, G. *et al*, 1993 : 98).

V: mstari H: kipande P: mguu W: watid yaani aina ya mfululizo wa silabi

S: silabi

# B. 1) **Mwundo wa mstari au ubeti katika Ushairi wa Kiajemi wa kiutamaduni**

- Bahari ya *e motaqāreb:*




V: mstari  H: kipande P: mguu S: silabi

# B. 1.) **Haiwezekani kutumia ruwaza hizo**

- Ruwaza hizo zinaundwa kabisa na uwezo wa kutofautiana silabi kutokana na urefu au ufupi wake
- Katika fonolojia ya Kiswahili na lahaja zake:
  - Hakuna tofauti hiyo kati ya silabi fupi na ndefu
  - Pia hakuna tofauti kati ya urefu wa vokali
  - Kwa hivyo haiwezekani kabisa
- **Lakini kwa nini ruwaza hizo zaendelea kutumiwa?**

# B. 1) **Mwundo wa mstari au mshororo katika Ushairi wa Kiswahili wa kiutamaduni**

- Bahari ya SHAIRI:




*Mshororo au mstari una vipande viwili vilivyo na hesabu ya silabi 6 au 8*

# Ubeti katika bahari ya SHAIRI

- Katika ushairi wa Kiswahili neno la ubeti **<u>si mstari</u>** lakini kikundi cha mistari au mishororo
- Mishororo pia inakatwa kutokana na njia zinazofuatiliwa na vina
- Vina na mizani (urefu wa vipande) vinategemea **silabi**



# B. 1) **Uarabu uko wapi katika Ushairi wa Kiswahili?**

- *Maneno mengi ya istilahi ya kishairi yana asili ya Kiarabu*

- *Neno la ubeti* linatokea *bayt* "nyumba, ubeti"
- *Neno la shairi* linatokea *shair "mshairi"*
- *Mstari, Vina, Mizani, Bahari yanatokea Kiarabu pia nk*

*Lakini si maneno yote pia mengi yana asili ya Kibantu…*

# Asili za istilahi ya ushairi

| Nomino | Kiarabu | Kibantu |
|---|---|---|
| Aina | + | - |
| Arudhi | + | - |
| Bahari | + | - |
| Diwani | + | - |
| Hisabu | + | - |
| Kifungu | - | + |

| Nomino | Kiarabu | Kibantu |
| --- | --- | --- |
| Kina | + | + |
| Kipande | - | + |
| Kiwango | - | + |
| Kituo | - | + |
| Kupindulia | - | + |
| Mizani | + | - |
| Mkondo | - | + |

| Nomino | Kiarabu | Kibantu |
|---|---|---|
| Mshororo ? Ar. *miṣrā’*; pers. *mesrāʕ* | | |
| Mstari | + | - |
| Mshuko | - | + |
| Shairi | + | - |
| Silabi | - | - |
| Ubeti | + | - |

# B. 2. Ruwaza zinazoundwa na kikazo

- Mwanzishi wa nadharia hiyo, Alice Werner:

  "(…), and the conclusion I am led to adopt is that the verse is measured by beats rather than by syllables (…)."
  (WERNER, A., 1917)
- Kama katika ruwaza za Kigiriki, Kiarabu na Kiajemi nadharia hiyo inapingana na nadharia ya kienyeji ambazo zimeshaeleza kwamba washairi wanatunga ubeti (verse) kwa kutumia vina na mizani yaani silabi kama msingi mkuu wa arudhi

# Matokeo yake

- Hesabu ya vikazo inabadilika kutoka mstari mmoja mpaka mstari mwingine wa utenzi mmoja
- Nadharia ya vikwazo katika ushairi inataka hesabu hiyo iwe sawa katika mistari yote, kwa hivyo nadharia imekosa
- Washairi wa Kiswahili wameshaeleza kuwa wanatunga kwa kutumia vina na mizani yaani msingi wa kisilabi

# Sababu za upungufu wa ajabu katika nadharia za wageni

- Ajabu ni kuwa makosa yanaendelea sheria za arudhi zikiwa zimeshaelezwa wazi kuanzia mwaka 1954
- Kwa mwandishi kama Shariff (1988) makosa makubwa kama hayo hayawezekani kutokana na watalaamu isipokuwa yanatendwa maksudi
- Tumeshanona katika historia kuwa nadharia fulani zakataa asili ya Kiafrika kwa mambo ya Kiustaarabu (mfano wa Great Zimbabwe)
- Sababu nyingine zipo: kuzungumza kuhusu vitu ambavyo havijulikani sana, kuzungumza bila kujua, majaribio kupinga uhalisi wa kitu fulani kugundua kitu kingine, *nk*.

# B. 4) **Misingi ya Arudhi ya Ushairi wa Kiswahili**

- Ubeti unaundwa na misingi minne:
- ***<u>vina</u>***
- ***<u>mizani</u>***
- ***<u>mishororo</u>***
- ***<u>vipande</u>***

(ABEDI, 1954; SHARIFF, 1988; KING'EI *et al,* 2001; ROY, 2013)

# C. **Kutoka Misingi mpaka Bahari**

1) Bahari

2) Mikondo

3) Mitindo na Aina

# C. 1. **Bahari**

- Idadi yake inaweza kubadilika?

a) Sheikh Nabhany wa Mombasa (1985) anasema kuna bahari 13 tu, idadi yake haiwezi kubadilishwa. Kwa maoni yake mashairi huru si mashairi.

b) Ibrahim Noor Shariff (1988) anafikiri kuwa idadi inategegemea uwezo wa akili ya mtu kwa hivyo inaweza kubadilika mshairi iwe Mswahili .

c) Sanaa ya Ushairi ina wenyeji wengi sasa. Si Waswahili Visiwani tu. Mathias E. Mnyampala aliumba bahari mpya akitunga kama mshairi wa kiutamaduni.

# C. 1. a.) **Bahari 13 za Ushairi wa kiutamaduni Mwambao:**

1) **WIMBO**
2) **SHAIRI**
3) **ZIVINDO**
4) **UTENZI, UTENDI**
5) **UTUMBUIZO**
6) **HAMZIYA**
7) **DURA MANDHUMA - INKISHAFI**
8) **UKAWAFI**
9) **WAJIWAJI**
10) **TIYANI FATIHA**
11) **WAWE**
12) **KIMAI**
13) **SAMA - MAHADHI - SAUTI**

# C. 2. Bahari ya UTENZI kwa herufi za Kiajemi: mstari mmoja wa vipande vinne ni ubeti mmoja

***Utenzi wa Mwana Kupona***

Tarehe: 1858

Mshairi: Mwana Kupona Binti Msham

Mahali: Lamu (Kenya)

SOAS Swahili Manuscripts



# C. 2. UTENZI na herufi za Kirumi: mistari minne ni ubeti mmoja

***Kimwondo #2***

Tarehe: 1975

Mshairi: Mahmud Ahmed Abdul Qadir « MAO »

Mahali: Lamu (Kenya)

ROY, M. 2013. Kiamu, archipel de Lamu. PAF. pp 174-175

***Présentation de la versification des strophes 75 et 76 du poème Kimwondo namba 'two'***

strophe (**ubeti**) n° 75

a: twaˈyuːa ˈkuːwa lɪˈsaː**nɪ** — " Nous savons que la langue "

twa-ˈyuː-a ˈkuː-wa lɪ-ˈsaː-**nɪ**
1 2 3 4 5 6 7 8

**mshororo** (pl **mishororo**): un vers composé, ici, de huit syllabes ou **mizani** (sg **mizani**)

b: hʊˈɟɛːpa ˈliːlo mɔˈyɔː**nɪ** — " Dérobe ce qui est dans le cœur "

c: akaˈnɛːna haðɪˈraː**nɪ** — " Et elle parle en public "

d: ɓiːla ˈwɛwɛ kʊrɪˈðiː**a** — " Sans que tu aies à donner ton avis"

**ubeti** (pl **beti**): strophe composée de quatre **mishororo** (a, b, c, d)

strophe (**ubeti**) n° 76

**kina** (pl **vina**): rime interne à **l'ubeti**, répétition de la syllabe finale des trois premiers **mishororo**

a: ˈhiːnɪ nɪˈkʰuːɓwa heˈkiː**ma** — " Ceci est une grande source de sagesse "

b: meˈwɛːka ˈmɔːla kaˈriː**ma** — " Que le Seigneur, le Généreux a placée "

c: mwaːna aˈɗaːmʊ kʊˈsɛː**ma** — " Que l'être humain dise "

**kikomo** (pl **vikomo**): "pause", ou quatrième et dernier **mshororo** (d) de chaque **ubeti**

d: lɪˈlɛː aloðamɪˈriː**a** — " Ce qu'il a l'intention de faire "

**bahari** (pl **bahari**): rime finale, ici, la voyelle **a** de la dernière syllabe qui se répète tout le long du poème à la fin du **kikomo** de chaque **ubeti**

# C. 2. Lakini ni bahari moja tu kwa sababu msingi wa vina unalingana kabisa






# C. 2. Mfululizo wa vipande vinne vyenye silabi 8 ni ubeti mmoja

**Utenzi wa Mwana Kupona (1858):**



- Strophe 1

1.Ne-ge-ma wa-ngu bi-n-ti

2.M-cha-che-fu wa sa-na-ti

3.U-pu-li-ke wa-si-a-ti

4.A-sa u-ka-zi-nga-ti-(y)a



- Strophe 2 (3 ktk. J.W.T ALLEN 1962)

1.Ndo-o mbe-e u-ji-li-si

2.Na wi-no na qa-ra-ta-si

3.Mo-yo-ni ni-na ha-di-thi

4.Ni-me-pe-nda ku-kwa-mbi-a

**Kimwondo #2 (1975):**

Strophe 75

Twa-yu-a ku-wa li-sa-ni

Hu-je-pa li-lo mo-yo-ni

A-ka-ne-na ha-dhi-ra-ni

Bi-la we-we ku-ri-dhi-(y)a

Strophe 76

Hi-ni ni ku-bwa he-ki-ma

Me-we-ka Mo-la Ka-ri-ma

Mwa-na A-da-mu ku-se-ma

Li-le a-lo-dha-mi-ri-(y)a

# C.2. UTENZI wa karne ya 16 na 19

- 1532 *Utenzi wa Fumo Liyongo*
- 1858 *Utenzi wa Mwana Kupona*
- Tenzi hizo mbili zenye arudhi sawa kupitia karne zilitungwa kwenye mahali ya Visiwa vya Lamu

# C.3. Bahari ya SHAIRI

- Idadi ya mistari katika ubeti mmoja haiwezi kupungua mistari minne
- Vina vya kati na vya mwisho vinakata vipande viwili katika kila mstari
- Kipande cha mwisho kabisa cha ubeti unaweza kuwa na kina kinacholingana popote katika vipande vya mwisho vya beti zote nyingine
- Katika ukurasa wa karatasi njia za vina zinachora mipango maalum inayounda aina au mtindo fulani vya mashairi

# KUPINDULIA 1

| KIBAYA KINA MWENYEWE | | LE MAUVAIS A UN PROPRIETAIRE |
|---|---|---|
| Nilikwenda ziwa Go**mbo**, | samaki wakavuli**we**, | Je suis allé au lac Gombo, et que les poissons soit pêchés, |
| Pamoja na changu cho**mbo**, | havue nifaniki**we**, | Avec mon bateau, qu'on ne les [littéralement qu'il ne NDT] pêche pas afin que je réussisse, |
| **/mbo/** | /we/ | |
| Nikasikia mafu**mbo**, | samaki kwitwa tumba**we**, | Puis j'entendis des énigmes, le poisson être appelé du corail, |
| Kibaya kina mwenye**we**, | ingawa chanuka sho**mbo**. | La mauvais a un propriétaire, quand bien même il pue l'odeur du poisson. |
| **8 syllabes** | **8 syllabes** | [les tracés des chaînes de rimes sont de nous NDT] |

# MSHUKO

| DAIMA PIMA UPEPO | | TOUJOURS PRENDS LA MESURE DU VENT |
|---|---|---|
| Kinga moto uwaka**po**, | na uzime uzima**po**, | Préviens là où s'allume le feu, et éteins où il s'éteint, |
| Zima hapo uanza**po**, | ni hatari uwacha**po**, | Eteins-le au début, c'est dangereux si tu le laisses, |
| Moto hauna mkwe**po**, **/po/** | pande zote uzinga**po**, **/po/** | Le feu n'a pas de moyen d'être évité, quand de tous côtés il fait le tour, |
| Chungua sana upe**po**, | ni wapi welekea**po**. | Regardes bien le vent, la direction dans laquelle il se dirige. |
| **8 syllabes** | **8 syllabes** | [les tracés des chaînes de rimes sont de nous NDT] |

# KUPINDULIA 2

| « MTOTO KUOMBA PESA | | L'ENFANT MENDIANT |
|---|---|---|
| Mabwana nawauli**za**, | jambo linalonita**sa**, | Messieurs je vous demande, une chose qui me cause du soucis, |
| Sijui ntawachuki**za**, | hutokea nikako**sa**, | Je ne sais si vous me détesterez, s'il s'avère que j'ai commis une faute, |
| **/za/** [8] | /sa/ | |
| Iwapo linapende**za**, | niambiwe kwa sia**sa**, | Si la chose vous plaît, répondez-moi par la politique, |
| Mtoto kuomba pe**sa**, | hii ni tabia ga**ni** ? | Un enfant qui mendie de l'argent, qu'est-ce que ce comportement ? |
| | **/ni/** | |
| **8 syllabes** | **8 syllabes** | |

[le tracé des chaînes de rimes est de nous NDT] »

# Bahari ya WIMBO na njia mbili za vina

*Huba na mapendi, yamezoningiya,*

*Hamu huitundi, hata saa moya,*

*Toba wangu kandi, huwat'i udhiya.*

Zena, 1966, Mombasa (Kenya)

WIMBO 3*(p=2|6,a-6,b#)

Modèle graphique

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1er vers/*mshororo :* | 6 syllabes,**a** | | 6 syllabes,**b#** | |
| 2ème vers/*mshororo :* | 6 syllabes,**a** | rimes internes | 6 syllabes,**b#** | rimes finales |
| 3ème vers/*mshororo :* | 6 syllabes,**a** | *vina vya kati* | 6 syllabes,**b#** | *vina vya mwisho* |
| | 1er hémistiche/*kipande* | | 2ème hémistiche/*kipande* | |

# Bahari ya WIMBO na njia tatu za vina

| | | |
|---|---|---|
| Huna ihisani | ungatendwa wema | hukumbuki |
| Hutundi huoni | mambo ya dhuluma | yenye dhiki |
| Nyonda huthamini | mbeko na heshima | huzitaki |

Nabhany, 1984, Mombasa (Kenya)



# Bahari ya WIMBO na njia nne za vina

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kukwepuka nana | sitaki | nasonona | ndani |
| Kusubiri tena | ni dhiki | muhibana | lini ? |
| Nyonda kuonana | ashiki | hali sina | shani |

Nabhany, 1983, Mombasa (Kenya)



# Bahari ya INKISHAFI ina njia ya viwango upande wa kushoto

19.

Dunia ni jifa siikurubu
Haipendi mtu ila kilabu
Ini hali gani ewe labibu
Kuwania mbwa hutukizwaye !

20.

Kamwe ina ila iliyo mbovu
Ilikithiriye ungi welevu
Ikalifu mno kutaka mavu
Kupa watu ngeya ikithiriye

**Nasir, Sayyid Abdallah bin Ali (1720-1820)**

# Bahari ya UTUMBUIZO haina mizani lakini ina njia za vina

- *«* […] *tumbuizo* […] *ni ya utungo ambao hauna hisabu maalumu ya mizani, lakini mwisho wa kila kifungu au mshororo humalizikia kwa kina. Utumbuizo wa aina hii huweza kuwa na kina kimoja au zaidi.* […] *»* (SHARIFF, I., N., 1988: 52)

# Muundo wa kihierarkia wa Misingi

- *Athari za misingi zinakuja moja baada ya nyingine kuzalisha ubeti:*



# D.
# Ushairi wa Mathias E. Mnyampala (1917-1969)

***Kuumba bahari na aina mpya za tungo kwa kuhifadhi kabisa sheria za kiutamaduni wa Ushairi wa Kiswahili***

# D. UTENZI unaolingana kabisa na tenzi za zamani: *Utenzi wa Zaburi*

| | |
|---|---|
| *Waisome walimwengu,* | Que les hommes les lisent, |
| *Wamhimidie Mungu,* | Qu'ils rendent gloire à Dieu, |
| *Muumba nchi na mbingu,* | Le Créateur du pays et du ciel, |
| *Aabudiwe Karimu* | Qu'Il soit vénéré le Généreux. |
| | |
| *Dibaji nimemaliza,* | L'introduction j'ai terminée, |
| *Naanza kuieleza,* | Je commence à l'expliquer, |
| *Msomaji tekeleza,* | Lecteur prends conscience, |
| *Haya ninotakalamu.* | De ces choses que j'écris. |
| | |
| *Ninaianza zaburi,* | Je commence les *Psaumes*, |
| *Kwa njia ya ushairi,* | Par le chemin de la poésie, |
| *Kama inavyohubiri,* | Comme il annonce , |
| *Kuwadibu wanadamu.* | Pour enseigner aux êtres humains. |

(MNYAMPALA, M., E., *c.*1965 : 9)

# D. **Mageuzo**

- Mageuzo yote yanafuata sheria za misingi ya ushairi wa kiutamaduni.
- ***Mathias E. Mnyampala anazalisha ushairi mpya akihifadhi kabisa ushairi wa kale!***
- Bahari mpya ya NGONJERA
- Mtindo mpya wa VIDATO
- Bahari mpya ya MSISITIZO

# D. Bahari ya NGONJERA kama Malumbano ya kishairi

| | |
|---|---|
| *MWANA* L'ENFANT | |
| •*Ala, hivyo baba kweli, mabepari ni mirija ?* | Et bien ! Ainsi c'est vrai père, les capitalistes sont des pailles à vin ? |
| •*Hujikusanyia mali, kwa sababu ya ujanja,* | Ils se récoltent les biens, en raison de l'astuce, |
| •*Uongo huzusha kweli, haki zetu kutupunja ?* | Le mensonge se dévoile vraiment, nos droits nous en priver ? |
| •*Azimio la Arusha, limeleta haki kweli.* | La déclaration d'Arusha, elle a apporté le droit vraiment. |
| *BABA* LE PERE | |
| •*Azimio lenye heri, mkono ninaliunga,* | La déclaration est heureuse, ma main je lui prête, |
| •*Alijalie Kahari, Rabi Mola Mwenye anga,* | Que Dieu la bénisse, le Puissant le Seigneur le Lumineux, |
| •*Tukayafyeke mapori, shoka mundu na mapanga,* | Et que nous allions défricher la brousse, hache faucille et machettes, |
| •*Azimio la Arusha, laneemesha taifa.* | La déclaration d'Arusha, fait prospérer la nation. |

# NGONJERA

- Bahari hiyo inachanganyisha vitu vinne:

1) Malumbano ya Kishairi ya Washairi kuanzia karne ya 19 [bahari ya MASHAIRI]
2) Ngonjera za Kigogo ambazo ni Mahakama ya kiutamaduni kule Ugogoni
3) Azimio la Arusha la 1967
4) Mchezo wa kuigiza kutoka Ulaya

# Habari kutoka miswada ya Mathias E. Mnyampala ambayo haijachapishwa

# Miswada

- Ilikuwa inahifadhiwa kwa makini na mtoto wa pili wa Mathias E. Mnyampala, Bw. Charles M. Mnyampala
- Niliigundua Dodoma mwaka 2007 nikiongozwa na Mugyabuso M. Mulokozi
- Niliruhusiwa kuinukulu yote kwa picha za kielektroni

# Aina za miswada

- Miswada ya ushairi ambayo haijachapishwa bado
- Pia kuna miswada muhimu ya siasa na dini kama *Azimio la Arusha na Maandiko Matakatifu*
- Ndani yake Mnyampala anadhihirisha utakatifu na msingi wa kidini wa Azimio la Arusha kupitia Biblia, Kurani, Veddha na Masomo ya Kibuddha

# Msimamo wa Julius K. Nyerere kuhusu mswada huo

- https://medihal.archives-ouvertes.fr/medihal-01052416

# Pia Mnyampala aliandika habari za maisha yake

- Mswada uliandikwa kwa mkono wake wakati akikomea mwisho wa uhai wake (1968-1969)
- Ulipigwa chapa mwaka 2013 na shirika langu Ufaransa baada ya muda mrefu wa saburi
- Jina lake *Maisha ni kugharimia*

# Maisha ni kugharimia




Kitabu hiki kwenye Google Books Tanzania: bonyeza hapa

# MASHAIRI ya VIDATO

genre <u>SHAIRI</u> (quatre vers à hémistiches octosyllabiques par strophe/*ubeti*)

strophe/*ubeti* 1

1er vers : KAMA watunga 'Vidato' | ya vina kuvibadili
1er hémistiche | 2ème hémistiche
2ème vers : Lugha uipambe vito | bora bora vya aali
8 syllabes (1) /to/ | 8 syllabes
3ème vers : HAKUNA mwingine mto | ububujao kuwili
4ème vers : KIONGOZI ndio mali | Jarida la Kiswahili /li/ (2)
(3) /li/

strophe/*ubeti* 2

1er vers : KAMA fawidhi fadhili | afadhiliye taifa
1er hémistiche | 2ème hémistiche
2ème vers : Kuandika Kiswahili | cha ufasaha na sifa
8 syllabes | 8 syllabes
3ème vers : HAKUNA kupita hili | kwa ukarimu wa dhifa
4ème vers : KIONGOZI ndio shufa, | Jarida la Kiswahili /li/ (2)
(3) /fa/

strophe/*ubeti* 3

1er vers : KAMA utapiga defa | gazeti lipi lapita
1er hémistiche | 2ème hémistiche
2ème vers : Kwa mpango na sahifa | tegemeo la UKUTA
8 syllabes | 8 syllabes
3ème vers : HAKUNA ila magofa | magazeti ya matata
4ème vers : KIONGOZI ndiye nyota | Jarida la Kiswahili /li/ (2)
(4) /ta/



# D. Bahari mpya ya MSISITIZO



# Chombo cha Taifa letu (J.K. Nyerere)

strophe/*ubeti* n

ligne/*mstari*[111] 1 : 8 syllabes,**a(n)**

ligne/*mstari* 2 : 8 syllabes,**a(n)**

ligne/*mstari* 3 : 8 syllabes,**b(n)**

ligne/*mstari* 4 : 8 syllabes,**b(n)**

ligne/*mstari* 5 : 8 syllabes,**c(n)**

ligne/*mstari* 6 : 8 syllabes,**c(n)**

*Chombo cha Taifa letu,*
*Si sawa na vya wenzetu,*
*Vyao vyataka Rubani,*
*Aushike usukani,*
*Awe na mabaharia,*
*Wanaomsaidia.*

*Na kiwe kina mafuta,*
*Ya kutosha kukivuta,*
*Au kiwe na makaa,*
*Kwani pia yanafaa,*
*Chombo kimekamilika,*

**TAMATI**

Asanteni sana.

©2014 Mathieu Roy

*Habari zaidi kuhusu mimi:*

http://www.doyoubuzz.com/mathieu-roy